East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 7, Issue 1, 2024
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Upambanuzi wa Mikakati ya Kitashtiti katika Vibonzo vya Kisiasa Vya Gado

*Kerryann Wanjiku Mburu[1*], Dkt. Sheila Wandera-Simwa, PhD[1] na Prof. Nabea Wendo, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Laikipia, S. L. P. 1100-20300, Laikipia, Kenya.
[*] ORCID: https://orcid.org/0000-0002-9566-1607; Barua pepe ya mawasiliano: kmburu@laikipia.ac.ke

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*08 Januari 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Vibonzo vya Kisiasa, Tashtiti, Mikakati ya Kitashtiti, Mtandao.*

## IKISIRI

Taalumu ya uchoraji na uchapishaji wa vibonzo vya kisiasa umekuwepo tangu karne ya kumi na nane. Saana hii huwavutia watafiti wengi kutokana na uwezo wake wa kusimba jumbe zisizoweza kusemwa wazi wazi. Ifahamike kuwa sifa kuu ya vibonzo vya kisiasa ni kuwa vinapaswa kuwa cheshi na vyenye tashtiti ndiposa viweze kuwasilisha masuala tata kwa njia ya kimzaha. Kutokana na hali hii, utafiti huu ulichunguza tashtiti katika vibonzo vya kisiasa vya Gado vilivyochapishwa katika mwaka wa 2017 kwenye tovuti yake. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kupambanua mikakati iliyotumika katika kuendeleza maudhui ya kitashtiti katika vibonzo vilivyoteuliwa. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Semiotiki iliyoasisiwa na Ferdinand De Saussure, na baadaye kuhakikiwa na Chandler na pia Wamitila. Mihimili ya nadharia hii ilitumika kuchambua mikakati iliyotumiwa na Gado katika vibonzo vyake kwa minajili ya kuendeleza maudhui ya kitashtiti. Utafiti huu ni ulikuwa wa kimaelezo na ulifanyika mtandaoni, pale ambapo mtafiti alipekua tovuti ya Gado (www.gadocartoons.com) na kuteua kimaksudi vibonzo vinane kutokana na jumla ya vibonzo ishirini vilivyokuwa vimechapishwa katika mwaka wa 2017. Uteuzi huu ulijikita katika vibonzo vilivyofungamana na madhumuni ya utafiti huu. Kwa jumla, utafiti huu ulidhibitisha kuwa mwanakibonzo Gado alitumia mbinu za lugha kama vile; kinaya, kejeli, metonimia, sitiara, analojia na mwingiliano matini kama mikakati ya kuibua kitashtiti katika vibonzo vyake. Vilevile, utafiti huu ulionyesha kuwa Gado alitumia ishara kama vile; matumizi ya rangi mbalimbali, pamoja na alama kama vile; heshtegi, mviringo na nyota kama mikakati ya kuibua tashtiti katika vibonzo vyake. Mwishowe, utafiti huu ulidhibitisha kuwa vibonzo vilivyochapishwa kwenye mtandao, vilidhihirisha uhuru na ukali mwingi katika usawiri wa masuala mbalimbali, jambo ambalo lilisaidia katika kufanikisha lengo kuu la tashtiti; ambalo ni ushambulizi unaochochea mabadiliko. Mwishowe, matokeo ya utafiti huu yalitarajiwa kuwanufaisha wanamawasiliano, wanasemiotiki na wasomi wa masuala ya kisiasa kwa kuwapa mtazamo mpya kuhusiana na matumizi ya maneno na ishara katika kusimba jumbe tata zinazochapishwa kwenye mtandao ambapo kuna uhuru mwingi wa kuelezea masuala tata bila kudhibitiwa.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685

**APA CITATION**

Mburu, K. W., Wandera-Simwa, S. & Wendo, N. (2024). Upambanuzi wa Mikakati ya Kitashtiti katika Vibonzo vya Kisiasa Vya Gado. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 11-27. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685.

**CHICAGO CITATION**

Mburu, Kerryann Wanjiku, Sheila Wandera-Simwa and Nabea Wendo. 2024. "Upambanuzi wa Mikakati ya Kitashtiti katika Vibonzo vya Kisiasa Vya Gado". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 11-27. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685.

**HARVARD CITATION**

Mburu, K. W., Wandera-Simwa, S. & Wendo, N. (2024) "Upambanuzi wa Mikakati ya Kitashtiti katika Vibonzo vya Kisiasa Vya Gado", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 11-27. doi: 10.37284/jammk.7.1.1685.

**IEEE CITATION**

K. W. Mburu, S. Wandera-Simwa & N. Wendo "Upambanuzi wa Mikakati ya Kitashtiti katika Vibonzo vya Kisiasa Vya Gado", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 11-27, Jan. 2024.

**MLA CITATION**

Mburu, Kerryann Wanjiku, Sheila Wandera-Simwa & Nabea Wendo. "Upambanuzi wa Mikakati ya Kitashtiti katika Vibonzo vya Kisiasa Vya Gado". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Jan. 2024, pp. 11-27, doi:10.37284/jammk.7.1.1685.

## UTANGULIZI

Tashtiti ni taalauma ambayo imekuwepo tangu karne ya tano na ilianza Ugirikini kisha ikasambaa hadi nchi zingine za ulimwengu. Tashtiti ni aina ya sanaa inayokebehi, kubeza, na kudhihaki watu, taasisi za kijamii, na za kisiasa. Ayodi na wenzake (2014) wanaelezea tashtiti kama mtindo ambao unaotumiwa na watunzi kuelezea yasiyoweza kuelezewa bila kumchukiza, au kumkera msomaji. Ayodi na wenzake (2014) wanadai kuwa historia ya tashtiti ni ndefu na imekuwepo katika tamthilia na ushairi wa magharibi kwa miaka mingi na wanatashtiti kwa kwanza duniani walikuwa ni pamoja na Aristophane, Horace na Juvenal. Kwa kiwango kikubwa watafiti wanakubaliana kuwa tashtiti ni mojawapo ya modi za ujielezaji iliyoibuka miaka mingi iliyopita, lakini cha kushangaza ni kuwa kufikia sasa bado hakujakuwa na maafikiano kuhusiana na maana ya dhana ya tashtiti.

Lichtenstein na Nitsch (2022), anafafanua tashtiti kama mfumo wa mawasiliano unaohusishwa na mashambulizi, kuhukumu, dhihaka, uchezi, na urejelezi wa desturi za kijamii. Kulingana na maelezo ya Litchtenstein, tashtiti inajihusisha na uhakiki na ushambulizi wa taasisi zinazoendeleza mamlaka kwenye jamii. Hivyo, ili kazi yoyote ile iweze kusemekana kuwa ni ya kitashtiti lazima ionekana kuwa inashambulia taasisi au mtu fulani. Kwa kawaida, tashtiti haiwezi kufaulu kivyake na aghalabu hutegemea mbinu zingine za lugha ili iweze kutambulika. Knight (2004), anaeleza kuwa tashtiti husawiri "ushambulizi wa ainasafu" ambapo mara nyingi huwa inafaulu kwa kujifanya kuwa kitu kingine. Aghalabu, tashtiti hutwaa, kumiliki na kunyonya tanzu zingine kama vile riwaya, hotuba, shairi au hata vipindi vya televisheni na katika hali hii tashtiti huchukuliwa kama kimelea.

Hali kadhalika, ni vyema kuelewa kuwa kwa muda mrefu kumekuwa na mgogoro kuhusiana na maana ya dhana tashtiti. Kuna wale wanaoshikilia kuwa tashtiti ni mtindo wa mawasiliano (Dorner na Porzelt, 2016), na wengine wanadai kuwa tashtiti ni utanzu (Declercq, 2018), lakini ufafanuzi ninaokubaliana nao ni wa Stinson (2019) anayedai kuwa tashtiti ni modi na wala si utanzu na inafanya kazi kwa kushambulia mtu, taasisi, au tabia. Vilevile, tashtiti ni aina ya maandishi au ishara ambazo ni za kimaksudi na huwa na lengo maalum ambalo mara nyingi huwa kukejeli au kukebehi. Hivyo, lengo kuu la tashtiti ni "ushambulizi" wa kimaksudi wenye lengo la kusababisha mabadiliko.

Peifer na Lee (2019) wanadokeza kuwa tashtiti ni taalamu ya kuzorongesha inayochochea mabadiliko katika mfumo wa kijamii na kisiasa kwa njia ya kimzaha. Hivyo, tunaweza kuchukulia tashtiti kama uhakiki wa kisiasa wenye mzaha na unaolenga kufichua upumbavu, na unafiki

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685

miongoni mwa viongozi, serikali au taasisi za kiserikali. Hivyo, ili matini yoyote ile iweze kusemekana kuwa ni ya kitashtiti, ni lazima iwe na msukumo wa kuleta mabadiliko ya aina fulani katika siasa au jamii.

Tangu enzi za kale, taalamu ya uchoraji wa vibonzo vya kisiasa imefungamanishwa na dhana ya tashtiti. Sanaa ya uchoraji wa vibonzo vya kisiasa iliibuka kutokana na haja ya kuelezea masuala changamano ya kisiasa kwa njia rahisi na yenye kunata shauku za umma (Salisu na Nuhu, 2016). Haya yanawezekana kutokana na uwezo wa vibonzo kufinya masuala changamano katika picha na maneno yanayoweza kueleweka kwa urahisi. Kwa kawaida inachukuliwa kuwa vibonzo vya kisiasa vinavyochapishwa katika magazeti au kwenye mitandao mbalimbali ni vya kitashtiti na lengo kuu la vibonzo hivi sio kuburudisha tu bali ni kuweka wazi uozo uliopo katika jamii na katika ulingo wa siasa. Lengo kuu la vibonzo vya kisiasa ni kutashtiti wanasiasa na kuwashawishi walengwa wa vibonzo vile kufuata mkondo wa mawazo ya mchora vibonzo. Kando na kushawishi umma, vibonzo vya kisiasa hunuia kuleta mabadiliko katika uwanda wa kisiasa na maisha ya wanajamii. Kwa kiwango kikubwa tanzu za fasihi na drama zimecheza nafasi kubwa katika kusogeza mbele taaluma ya tashtiti, hata hivyo, vibonzo viliibua sifa mpya ya tashtiti kwa kufungamanisha jumbe zilizobeba uzito ndani ya nyembo finyu ya michoro au picha. Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu vibonzo vya kisiasa na athari zake kwa umma na hata zingine za kudhibitisha kuwa vibonzo vya kisiasa ni vya kitashtiti (Mulanda na Telewa 2014, Ng'etich 2020). akini utafiti huu ulidhamiria kuchunguza mbinu mbalimbali zilizotumiwa na mchora vibonzo maarafu Godfrey Mwapemba almaarufu Gado, na hasa vile alivyochapisha katika tovuti yake ya www.gadocartoons.com

## MAPITIO YA MAANDISHI

Sani (2014) walichunguza kuhusu uundaji wa tashtiti katika vibonzo vya magazeti nchini Nigeria. Mtafiti huyu alichunguza maneno yaliyotumika kwenye vibonzo vya kisiasa vya nchi ya Nigeria, kwa kuunda topoi za kileksia kwa minajili ya kutambua vipengele vya kileksia na matumizi yake katika matini zilizotumika katika vibonzo vile. Wataalamu hawa walidhihirisha kuwa, wanavibonzo wa Nigeria hutumia vihisishi kuwatashtiti viongozi wa kisiasa. Japo, utafiti wa Sani na wenzake ulitoa mchango mkubwa katika utafiti huu kwa kuonyesha jinsi vihisishi vinavyotumika katika uundaji wa tashtiti, utafiti wa Sani uliwacha pengo la kiusomi kwa kuwa ulijikita kwenye uhakiki wa matumizi ya lugha katika vibonzo. Pengo ambalo mtafiti alikusudia kuziba kwa kuhakiki ishara zote za kiisimu (michoro na maneno) katika uendelezaji wa tashtiti.

Kwa upande mwingine, Al- Momani na wenzake (2017) walifanya uhakiki wa kisemiotiki wa vibonzo vya kisiasa vilivyochapishwa nchini Jordan baada ya mwamko wa mwaka wa 2011 kule Uarabuni. Utafiti wao ulidhihirisha kuwa vibonzo vilivyochapishwa katika kipindi hiki, vilitumia mbinu za lugha kama vile; ucheshi, mchezo wa maneno, polisemia, mwingiliano matini, ubadili msimbo, udokezi na ukopaji kutoka kwa utamaduni ili kukejeli na kutashtiti uongozi na hali ya kisiasa nchini Jordan. Utafiti huu wa Al-Momani na wenzake ulifanana kwa kiasi kikubwa na utafiti huu lakini tofauti iliyopo ni kuwa; katika uchunguzi wao watafiti hawa walitafitia mikakati ya lugha na ishara zilizotumika katika maudhui yaliyojitokeza katika vibonzo vilivyoteuliwa.

Kando na hayo, Kondowe na wenzake (2014) walichunguza jinsi sifa za kunenwa na zisizo za kunenwa katika vibonzo vya kisiasa vinavyotumika katika kusawiri viongozi wa kisiasa nchini Malawi. Utafiti wao ulidhihirisha jinsi wanavibonzo huvunja, kupuuza au kutofuata kanuni shirikishi za mazungumzo katika uangaziaji wa masuala ya kisiasa nchini Malawi. Matokeo ya utafiti wao, yalidhihirisha kuwa wanavibonzo huvunja kanuni shirikishi za mazungumzo kwa minajili ya kutashtiti taasisi za mamlaka na kama mkakati wa kuepuka hali ya kutoa makataa na kama mbinu ya kuifanya hadhira yao kuunda uelewa wao kuhusiana na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685

masuala ya kisiasa nchini mwao. Kwa kiasi kikubwa, utafiti wa Kondowe na wenzake ulitoa mwongozo katika utafiti huu, utafiti wao ulitofautiana kwa kiasi kikubwa na utafiti huu kwa kuwa ulijikita katika kuchambua sifa za kiisimu zilizojitokeza kwenye vibonzo vya kisiasa mintarafu ya kanuni shirikishi za mazungumzo za Grice, ilhali utafiti huu ulijikita katika uchambuzi wa kisemiotiki wa vibonzo vya kisiasa kwa minajili ya kutambua mikakati ya kitashtiti iliyotumika katika vibonzo ili kuvifanya viwe vya kitashtiti.

Katika utafiti wake Eko (2015) alichunguza suala ya uhamiaji wa vibonzo vya magazeti kutoka kwenye magazeti na majarida yanayomilikiwa na kampuni fulani za utangazaji hadi kwenye mitandao ya kijamii na tovuti za kibinafsi. Mtafiti huyu alidai kuwa kwa muda mrefu vibonzo vya kisiasa vilichapishwa kwenye magazeti na majarida kama njia ya kuwasilisha hoja ambazo kwa kawaida ni vigumu kuwasilishwa kwa njia iliyo wazi. Hata hivyo, kutokana na utandawazi na harakati za kutafuta uhuru wa kujieleza, baadhi ya wanavibonzo wamebadili mkondo na kuanza kuchapisha vibonzo vyao katika mitandao yao ya kibinafsi. Uchunguzi wa Eko (2015) ulidhibitisha kuwa wanavibonzo wa Kiafrika wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira yenye uhasama na udhibiti mkubwa kutoka kwa serikali, pamoja na mashirika ya magazeti nchini. Kutokana na hali hii, wengi wao wamemudu hali ya kujidhibiti wenyewe. Hata hivyo, kwa wale ambao kazi zao zinaonekana kana kwamba zinashtumu taasisi zinazoendeleza mamlaka, wao hujaribu kudhibitiwa na wakati mwingine wanaweza kufunguliwa mashtaka na kufungwa gerezani. Eko aligundua kuwa udhibiti na uhasama huu, hupelekea wanavibonzo wengi kubadili modi ya kuchapisha vibonzo vyao kutoka magazetini; ambapo kuna udhibiti mkubwa hadi mtandaoni ambapo kuna uhuru mkubwa wa kujieleza. Utafiti huu wa Eko (2015), ukajenga msingi dhabiti ambamo mtafiti alijengea uchunguzi wake.

## MSINGI WA NADHARIA

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Semiotiki iliyoasisiwa na mwanaisimu wa Kiswisi Ferdinand de Saussure katika mwaka wa (1857-1913) na baadaye ikaendelezwa na wanafalsafa Charles Pierce (1958) pamoja na wahakiki kama vile Umberto Eco na Roland Barthes (1973). Baadaye nadharia hii iliangaliwa upya na wataalamu kama vile Chandler (2002) na Wamitila (2002). Nadharia hii ilichukuliwa kuwa faafu zaidi katika kuhakiki ishara mbalimbali zilizojitokeza katika vibonzo vya kisiasa kwa minajili ya kuchunguza mikakati iliyotumika katika kuibua tashtiti katika vibonzo vilivyoteuliwa.

Nadharia ya Semiotiki ilifaidika pakubwa kutokana na mawazo ya mwana- isimu wa Kiswizi Ferdinand de Sasssure kuhusiana na ishara. Chandler (2002) alieleza kuwa Saussure alifafanua ishara za kiisimu kama zile zilizo na viambajengo viwili kiashiria na kiashiriwa. Ambapo kiashiria ni kile kinachoonekana, kusikika au kugusika na kiashiriwa ni picha zinazojitokeza akilini tunapoona, kusikia au kugusa kitu; yaani dhana ambayo ishara inawasilisha. Kulingana na Saussure, ishara zote zinazotumika ni za kinasibu tu na hakuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya ishara na maana zake.

Wamitila (2002) alifafanua kuwa ingawaje nadharia ya Semiotiki ilichota mawazo yake kutoka kwa Saussure na Pierce, kuzuka kwa nadharia hii kulihusishwa na kipindi cha miaka ya 1970 na mawazo ya Roland Barthes yalitoa mwongozo dhabiti kuhusiana na uchambuzi wa ishara. Chandler (2002) alielezea kuwa Barthes aliamini kuwa maana za kitamaduni huwa zimejikita katika lugha husika. Mtazamo wake ulihusisha dhana ya udokezi ama kama anavyoeleza; maana ya ziada. Kulingana na Barthes, kiashiriwa kinaweza kuwa kiashiria katika kiwango kingine cha maana. Kwa mfano istilahi “nyekundu” humaanisha aina fulani ya rangi, lakini pia inaweza kudokeza “hatari” katika utamaduni wa Kiafrika.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685

Wamitila (2002), alieleza kuwa Barthes aliangazia misimbo mitano ya usomaji ambayo iliwacha athari kubwa katika uhakiki wa ishara na uashiriaji. Kulingana na mhakiki huyu, matini yoyote ile inapaswa kuvunjwa katika vitengo vidogo vidogo ili kusaidia katika ufasiri wake. Misimbo hii ilichukuliwa kama mihimili au nguzo kuu za nadharia ya semiotiki. Barthes alifafanua misimbo hii kama ifuatavyo:

- Msimbo wa matukio ambao ulihusu namna matukio yanayopatikana na kufuatana katika kazi yoyote ile ya kisanaa na jinsi msomaji anavyounda na kuuelewa msuko wa kazi hiyo ya kisanaa kwa kutathmini jinsi matukio yanavyofuatana kiathari au ki-sababishi. Katika utafiti huu, mhimili huu ulimsaidia mtafiti katika kueleza na kufafanua matukio yaliyojitokeza katika vibonzo vya kisiasa vya Gado vilivyoteuliwa kwa minajili ya kuhakiki ishara zilizojitokeza.

- Msimbo wa kihemenitiki unahusu taharuki au usimulizi. Aghalabu msimbo huu huitwa msimbo wa kusimulia au msimbo wa kutamba hadithi na unaweza kufumbatwa kwenye anwani ya kazi fulani. Mhimili huu, ulimwongoza mtafiti katika kuelewa yaliyomo kwenye vibonzo alivyoteua kwa kuangazia vidokezo vilivyojitokeza katika anwani za vibonzo vilivyoteuliwa. Kutokana na anwani za vibonzo vile, mtafiti aliweza kujiuliza maswali yaliyojenga taharuki ya kutaka kuhakiki vibonzo vile kwa minajili ya kuelewa ujumbe uliojitokeza.

- Msimbo wa ki-seme hueleza elementi nasibishi za kisemantiki ambazo hutupa picha ya mhusika au matukio fulani katika kazi za kisanaa kutokana na viashiria katika kazi zile. Kutokana na mhimili huu, mtafiti aliweza kutathmini ishara zilizokuwepo katika vibonzo vilivyoteuliwa na akaweze kuelezea picha zilizojitokeza akilini mwake kama mhakiki wa vibonzo vile.

- Msimbo wa kiishara unahusishwa na namna wasomaji wanavyovumbua maana za ishara katika kazi za kisanaa. Msimbo huu wa kiishara ulikuwa kidokezo kikuu katika kuchanganua ishara kama zilivyojitokeza katika vibonzo vya kisiasa. Katika utafiti huu, mhimili wa msimbo wa kiishara ulimsaidia mtafiti katika kuelezea maana ya ishara zilizokuwepo katika vibonzo vilivyoteuliwa kama vile, rangi zilizotumia, ukubwa wa maneno yaliyotumiwa, kimo cha watu waliosawiri katika vibonzo vile pamoja na mitindo ya lugha katika vibonzo vile.

- Msimbo wa kirejelezi hujengwa kutokana na viashiria vya kiutamaduni ambavyo vinarejelewa katika kazi za kisanaa. Huhusisha matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na hivyo kuipa kazi fulani nguzo ya kiutamaduni. Msemaji akisema kuwa anakielewa kitu anachokimaanisha msanii husema hivyo katika msingi wa kiurejelezi au kiutamaduni. Mhimili huu, ulimwongoza mtafiti katika kuelewa matukio na jumbe zilizosimbwa katika vibonzo vilivyoteuliwa. Hili lilifanyika kwa kuhusisha utamaduni na mazingira ya mchora vibonzo na jumbe zilizojitokeza katika vibonzo vile kwa minajili ya kufasiri na kuhakiki jumbe kama zilivyokusudiwa na mchora vibonzo.

Kwa jumla, utafiti huu uliongozwa na mihimili yote mitano ya nadharia ya kisemiotiki. Mtafiti alitumia kila mhimili kuchambua matukio yaliyojitokeza katika vibonzo vilivyoteuliwa, kisha akahakiki na kutolea maelezo ishara zilizojitokeza katika vibonzo vile. Mwishowe, nadharia hii ilimsaidia mtafiti kufafanua maana zilizotokana na ishara zilizokuwepo katika vibonzo vile na maana hizi ndizo zilizoibua suala la tashtiti.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulifanyika mtandao na maktabani ambapo mtafiti alidurusu vitabu, magazeti, na tafiti za wengine zilizohusiana na mada ya vibonzo vya kisiasa na tashtiti. Kwa kuwa data ya utafiti huu ilikuwa vibonzo vya kisiasa vilivyochapishwa na Gado, mtafiti alipekua tovuti ya Gado (www.gadocartoons.com) na akapakuwa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685

vibonzo vinane vilivyochapishwa katika mwaka wa 2017 na hasa vilivyohusu nchi ya Kenya na vilivyooana na malengo ya utafiti huu. Muundo wa utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo ambapo mtafiti alifafanua yale yaliofungamana na uhakiki na uchambuzi wa vibonzo vilivyoteuliwa. Mtafiti alichagua vibonzo vilivyochapishwa katika kipindi cha 2017 na hasa vilivyohusu nchi ya Kenya kwa kuwa kulikuwa na uchaguzi mkuu baada ya miaka mitano ya kuanzishwa kwa serikali za kaunti na mengi yalikuwa yametendeka nchini Kenya, tangu mfumo wa serikali za kaunti kuanzishwa katika mwaka wa 2013. Hivyo, mtafiti alichukulia kuwa vibonzo hivi vingesheheni utendakazi wa serikali ya wakati huo katika muhula wao wa kwanza na kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2017 katika mfumo wa ugatuzi. Sampuli ya utafiti huu ilisheheni data pana ya vibonzo ishirini vilivyohusu nchi ya Kenya, na vilivyokuwa vimechapishwa kwenye tovuti ya Gado. Baadaye mtafiti alichuja data yake na kuteua vibonzo vinane ambavyo alivipakuwa kwa minajili ya utafiti huu, uteuzi huu uliongozwa na madhumuni ya utafiti huu.

## MATOKEO YA UTAFITI

Utafiti huu ulilenga kupambaua mikakati ya kitashtiti katika vibonzo vya kisiasa na hasa vibonzo vya mwanavibonzo maarufu Gado na hasa vile alivyochapisha katika tovuti yake. Kwa muda mrefu, vibonzo vya kisiasa vimekuwa vikichapishwa kwenye magazeti na majarida lakini kutokana na utandawazi na udhibiti ulioko kwenye magazeti, wanavibonzo wengi wameamua kuchapisha vibonzo vyao katika mitandao yao ya kibinafsi ambako kuna uhuru mwingi wa kujieleza.

Kama ilivyodokezwa awali, kumekuwa na migogoro kuhusiana na upambanuzi wa dhana ya tashtiti (Griffin, 2015). Kwa kifupi wataalumu wengi wamekubaliana kuwa ufafanuzi wa tashtiti ambao unaweka wazi masharti na hali toshelevu ya jambo kutambulika kama la kitashtiti haiwezekani (Declerq, 2018). Hata hivyo, wataalamu wameamua kufafanua tashtiti kwa kuangalia sifa bainifu za tashtiti kupitia ufananao wa kifamilia na vishada visivyokuwa na sifa muhimu (Condren, 2023). Kwa mujibu wa utafiti huu, mtafiti alichukulia tashtiti kama dhana yenye sifa ya kuhakiki, kuburudisha na pia yenye nia ya kuleta mabadiliko. Hivyo, mtafiti akaongozwa na maelezo ya Knight (2004), kuwa tashtiti husawiri "ushambulizi wa ainasafu" ambapo mara nyingi huwa inafaulu kwa kujifanya kuwa kitu kingine, na hivyo tashtiti hutegemea mbinu zingine za lugha na ishara ili ijitokeze. Hivyo, makala haya yalichunguza mtindo ya lugha kama vile; kinaya, kejeli, analojia, metonimia, sitiara na mwingiliano matini pamoja na ishara kama vile; matumizi ya rangi kama mkakati iliyotumia na Gado kuvifanya vibonzo vyake kuwa vya kitashtiti.

### Sitiari

Sitiara ni mbinu inayotumia kitu kimoja kurejelea kitu kingine. Kwa kifupi, sitiara ni mbinu ya kutumia mfanano uliopo baina ya vitu kwa minajili ya kutumia dhana moja kurejelea dhana nyingine na hapa ndipo uhamishaji wa maana hujitokeza (Kahiga 2020). Kwa mujibu wa utafiti huu, mtafiti alitumia dhana ya sitiara kumaanisha ulinganisho wa vitu viwili ambapo maneno hayajatumika lakini ni wa "kuonekana" kupitia michoro au picha. Mwanavibonzo Gado, alitumia sitiari kutoa ulinganisho baina ya vitu kwa minajili ya kukejeli au kukebehi wahusika waliosawiriwa katika vibonzo vile. Kutokana na hali hii, Gado alionekana kuwa kebehi, shambulia na kuwahakiki wahusika katika vibonzo hivi kwa minajili ya kufichua ufisadi, unafiki, au uongozi mbaya.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685

**Kibonzo 1: $K_1$UKS Kampeni za NASA**




Kutoka: (**http://gadocartoons.com/nasa-and-their-campaign/**)

Kwa mfano, katika Kibonzo $K_1$UKS, msanii anatuonyesha taswira ya vinara wa muungano wa NASA, ambao walikuwa wapinzani wa serikali ya Jubilee nchini Kenya katika kinyang'arinyo cha urais. Viongozi hawa wamechorwa wakiwa wamekwea mlingoti uliandikwa *Flag Bearer* na chini ya mlingoti ule kuna mtego ulioandikwa NASA na ndani kuna onekana mchoro ambao mtafiti alichukulia kuwa ni wa kuku aliyeiva na aliyeandikwa *Govt Posts* na anonekana akitoa harufu nzuri. Hali ya msanii kufananisha ahadi ya nyadhifa za serikali kama kuku aliyeiva na anayetoa harufu nzuri, inaibua sitiara. Kando na hayo, Gado anapotusawiria mtego uliandikwa NASA na mtego ule umefungiliwa mlingoti uliokwewa na vinara wengine wa muungano wa NASA, alikuwa anapitisha ujumbe kuwa kuungana na muungano wa NASA ni mtego ambao utanasa yeyote anayetaka kujiunga nao. Hali ya msanii kufananisha kuku na nyadhifa za serikali na muungano wa NASA na mtego ni sitiari. Cha muhimu ni kuwa msanii, alitaka kuonyesha kuwa viongozi hawa wa muungano wa NASA walikuwa walaghai na walikuwa wanajaribu kulaghai wengine wajiunge na chama chao ingawaje wao wenyewe hawakuwa wamejipanga.

Kwa mujibu wa nadharia ya semiotiki na hasa mhimili wa kiishara kama ulivyoelezwa na Wamilita (2002), kwa kawaida, unapotaka kumshika panya kwenye mtego, huwa unateka nathari yake kwa chakula kinachotoa harufu nzuri, ndiposa aingie kwenye mtego. Vivyo hivyo, msanii alitumia ishara ya mtego, uliokuwa na kuku aliyetoa harufu nzuri na ulioandikwa NASA, kuwatega wanasiasa waliolaghaiwa kujiunga na muungano wa NASA, huku wakiwa na matumaini kuwa wangepata nyadhifa mbalimbali ambazo kwa hakika viongozi wa NASA hawakuwa nazo. Basi, msanii alikuwa anamaanisha kuwa viongozi hawa wa NASA walikuwa walaghai na alikuwa anawatashtiti, jambo ambalo kwa kawaida hangelisawiri kwa wazi ikiwa alikuwa anachapisha kibonzo hiki kwenye magazeti au televisheni, lakini kutokana na uhuru alioupata kutokana na kutumia tovuti yake binafsi, aliweza kusawiri masuala kama alivyoyaona bila kudhibitiwa. Katika kibonzo hiki, msanii alitumia mbinu ya stiara kukebehi ulaghai wa viongozi wa muungano wa NASA na hivyo kuwatashtiti

**Kejeli**

Kejeli ni dhana inayodokeza unyume katika usemi, hali au tukio. Kando na hayo, Baraza la

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685

Kiswahili la Zanzibar (2010), linaeleza kejeli kama neno au tendo la kuonyesha dharau kwa mtu. Vilevile, Mbatia (2001) anaelezea kejeli kama mbinu inayotumiwa katika matamshi na nia kuu ni kuchoma, kukata na kutia uchungu. Hivyo, kutokana na maelezo haya na ufafanuzi tulitoa awali wa dhana ya tashtiti kama mbinu inayolenge kukebehi au kukejeli kwa minajili ya kuleta mabailiko, utafiti huu uligundua kuwa msanii Gado alitumia kejeli katika kuibua tashtiti katika vibonzo vyake kama inavyodhihirika katika mfano huu

**Kibonzo 2: $K_1$UO, Jubilee italeta Maziwa na Asali**




Kutoka: (**http://gadocartoons.com/Jubilee-will-bring-milk-honey**).

Katika kibonzo hiki, kejeli inajitokeza kupitia maneno haya;

> *Forget Water...Jubilee Will Bring Milk and Honey to You. Just Remember...Kura Yako, Haki Yako!!* [Sahau Maji .... Jubilee Itawaletea Maziwa Na Asali. Kumbuka Kura Yako, Haki Yako]

Kama tulivyokuwa tumeeleza awali kuwa kejeli ni hali ya unyume, tukilinganisha matukio katika kibonzo $K_1$UO na maneno yanayotamkwa na rais na naibu rais wa nchi ya Kenya wa wakati huo, basi hali ya unyume inajitokeza. Katika kibonzo hiki, msanii Gado ametusawiria mizoga na mafuvu ya binadamu na wanyama kuashiria kuwa binadamu na wanyama wamekwisha kufa wakingoja viongozi waliowachagua wawaletee mahitaji yao ya kimsingi kama maji na chakula. Katika kibonzo kile, Gado anatuchorea makopo yaliyo pembeni mwa kibonzo $K_1$UO kuonyesha kuwa watu waliokufa walikuwa tayari na makopo ya kutekea maji. Hivyo, msanii anapotuonyesha rais na naibu rais wakiwambia "wananchi" ambao amekwisha kufa kutokana na njaa na ukosefu wa maji kuwa wasahau kuhusu maji, na kwamba serikali ya Jubilee itawaletea maziwa na asali anawatashtiti viongozi hawa kwa kutowajali wananchi. Kutokana na matamshi ya rais na naibu rais, tunagundua kuwa msanii anatumia mbinu ya kejeli kushambulia na kuhakiki tabia ya viongozi hawa ya kutowajali wananchi waliowapigia kura. Hivyo, msanii Gado anaonekana kuwa ametumia mbinu ya kejeli kuibua tashtiti katika kibonzo hiki.

## Kinaya

Mara nyingi dhana ya kinaya na kejeli huchukuliwa kama visawe na dhana hizi mbili zinachukuliwa kuwa zinaukuruba. Hata hivyo, Kamusi ya Kiswahili ya Karne ya Ishirini na Moja inafafanua kinaya kama hali ya kukinai au ni kinyume cha jambo. Mbatia (2001), anaelezea

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685

kuwa kinaya pia inakujulikana kama stihizai na hutumika kuonyesha utata wa maisha kwa kuweka wazi pengo lililopo baina ya mambo yanavyoonkena na jinsi yalivyokatika kazi za kitashtiti. Mtafiti aligundua kuwa msanii ametumia kinaya kama mkakati wa kutashtiti aidha viongozi au taasisi ambazo zinaendeleza mamlaka. Kwa mfano, katika kibonzo $K_1$UF msanii atumia mbinu ya kinaya kuonyesha pengo lilipo kati ya hali halisi na jinsi ilivyosawiriwa kwenye kibonzo kile.

**Kibonzo 3: $K_1$UF Kongamano la ugatuzi la mwaka wa 2017**

Kutoka: (**http://gadocartoons.com/devolution-conference-2017/**).

Katika kibonzo hiki, msanii atusawiria kongomano la nne la ugatuzi nchini Kenya, na katika kibonzo kile kunaonekana ndege nyingi zinazopaa angani na tunaonyeshwa mwanamke mmoja akimwambia mwanaume mwenzake;

> *Ooh We Are Making Progress…Before They Used to Arrive in Cars!* [Aah Tunapiga Hatua…Hapo Mwanzoni Walikuwa Wanawasili Kwa Magari!]

Matamshi ya wahusika hawa wawili wanaochukuliwa kuwa wanasimamia wananchi, unadhihirisha hali ya unyume. Kwa kawaida maendeleo ya nchi yoyote ile hupimwa kwa kuangalia ubora wa hali ya maisha ya wananchi na ikiwa maisha ya mwananchi wa kawaida yameimarika. Hivyo, msanii anpotusawiriwa taswira ya maendeleo yakipimwa kutokana na kuendelea kwa viongozi wanaoishi maisha ya hali ya juu, huku wananchi wa kawaida akitaabika, basi hicho ni kinaya. Hivyo, msanii alitumia mbinu ya kinaya kutashtiti hali ya wanasiasa kuinua hali yao ya maisha badala ya kuzingatia maslahi ya wananchi waliowachagua kuwawakilisha katika bunge au seneti.

**Metonimia**

Metonimia inaweza kuelezewa kama uwakilishaji wa neno au dhana moja na dhana nyingine ambayo inauhusiano fulani nayo. Gamen (2022) anaeleza metonimia kama uhusiano ambao dhana moja husimamia dhana nyingine ambayo ina ukaribiano mkubwa na hutumika badala ya kitu kingine ambacho kinahusiana nacho. Kwa kifupi, metonimia hujitokeza pale ambapo kuna uhamishaji wa maana kwa misingi ya ushirika. Vilevile, tunweza kusema ni kutajia kitu au wazo kwa jina la kingine ambacho kina uhusiano nacho. Katika utafiti huu, iligunduliwa kuwa msanii alitumia mbinu ya metonimia kama njia ya kutajia asiyoweza kutajwa kwa uwazi na pia kama mbinu ya kutashtiti viongozi na taasisi za kimamlaka kama inavyodhihirika katika mfano huu;

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685

**Kibonzo 4: $K_2$UO, Utekelezaji wa Ajenda ya Jubilee**




Kutoka: (**www.Gadocartoons.com**)

Katika kibonzo hiki tunasawiriwa aliyekuwa rais wa Kenya katika kipindi hicho akiwa amevalia sare rasmi ya majeshi, taji la ufalme kichwa na kwenye mkono wa kulia amebeba fimbo inayofanana na fimbo ya mamlaka ya spika wa bunge. Kwenye mkono wa kushoto kuna kikaragosi kidogo kilichovalia sare za askari na bunduki mkononi. Nyuma ya rais tunaonyeshwa akiyekuwa kinara wa wengi mbungeni na naibu rais wa wakati huo. Kinara wa waliowengi mbungeni anaonekana akiwa ameshika orodha fulani anayoisoma naye naibu rais anaonekena akichezesha kikaragosi mwenye sura ya nguruwe. Katika kibonzo hiki metonimia inajitokeza katika usawiri wa rais. Si jambo geni kwa marais wa nchi ya Kenya kuvalia sare rasmi za kijeshi kwa kuwa kulingana na katiba ya nchi ya Kenya, rais ni komanda mkuu wa majeshi ya nchi ya Kenya. Lakini jambo la kushangaza ni usawiri wa rais akiwa amevalia taji la kifalme ilhali nchi ya Kenya sio himaya bali ni nchi ya kidemokrasia inayoongozwa na rais anayechaguliwa na wananchi wenyewe. kando na hayo, tunaonyeshwa rais akiwa amebeba fimbo ya mamlaka ya bunge ambayo huashiria mamlaka ya spika wa bunge na mamlaka ya bunge. Hivyo, Rais akisawiriwa akiwa amebeba fimbo ile ni ishara kuwa amechukua mamlaka ya bunge ambayo ni kinyume na sheria ya nchi ya Kenya. Msanii anapotusawiria rais ambaye ni komanda mkuu wa majeshi, kisha ni mfalme, na anamamlaka juu ya bunge na tena polisi ni vikaragosi wake, basi tunachorewa taswira ya rais ambaye ni dikteta. Kwa kifupi, msanii ametumia metonimia kuhamisha maana kuwa rais wa wakati huo alikwa dikteta kwa minajili ya kumtashtiti na kumkebehi kwa tabia yake ya kutupilia mbali uhuru wa bunge na mahakama ya nchi ya Kenya. Katika mfano huu, usawiri wa rais ulikuwa metonimia iliyotumika kukashifu rais kwa kuwa dikteta.

## Analojia

Mwetulundila na Kangira (2015) wanaelezea analojia kama mlinganisho au mfananisho wa vitu viwili ambavyo havifanani lakini vina sifa au hulka zinazolandana kwa kiasi fulani. Hivyyo, tunaweza kufafanua analojia kama mlinganisho katika baadhi ya vipengele vya vitu viwili tofauti lakini kwa nia ya kuonyesha kuwa kunaweza kuwa na mfanano wa kiwango fulani. Katika utafiti huu, mtafiti aligundua kuwa msanii Gado

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685

ametumia mbinu hii ya analojia, kuibua tashtiti kwa kufananisha mambo ambayo haya fanani kwa minajili ya kuhakiki viongozi na taasisi za uongozi. Kwa mfano katika kibonzo $K_2$UWW, msanii analinganisha uhusiano kati ya madaktari wa nchi ya Kenya na ndoa yenye manyanyaso.

**Kibonzo 5: $K_2$UWW. Madaktari dhidi ya Serikali- Ndoa ya unyanyasaji**

Kutoka: (**http://gadocartoons.com/doctors-vs-govt-abusive-marriage/**).

Katika Kibonzo hiki msanii anatujengea taswira ya rais wa wakati huo akimchapa mwanamke aliyevalia nguo zilizoandikwa *Doctors*. Nyuma ya rais tunaona taswira ya naibu rais akiwa ameshikilia taji la ufalme la rais na nyuma yake kuna watu wawili. Mmoja wao hatuonyeshwi uso wake na mwingine ana uso wa paka. Kwenye upande wa kushoto wa kibonzo hiki, kuna Imam na mtu anayechukuliwa kuwa mchungaji kutokana na mavazi yake. Nyuma ya mchungaji na Imam kuna umati unaoonekana kustaajabika.

Kwenye upande wa kushoto wa kibonzo hiki, msanii anatuonyesha taswira ya mwanamke akisema;

> *It has been an abusive marriage* (hii imekuwa ndoa ya unyanyasaji)

Naye Rais anaonekana akijibu,

> *Stay out of this, let me sort her out!* (msijihusishe na haya, wacheni ni mshughulikie!)

Kwa kawaida, katika jamii nyingi wanawake hufanya kazi ya kutunza familia zao. Hivyo, msanii anapowasawiri madaktari kama mwanamke anapitisha ujumbe kuwa kazi ya madaktari ni kuwajali na kuwatunza wagonjwa. Hata hivyo, msanii anapomsawiri rais akimchapa mwanamke na kuwaonya watu wasiingilie mambo yao kwa kuwa anataka kumshughulikia mwanamke yule kwa kumchapa, msanii anapitisha ujumbe kuwa uhusiano kati ya rais na madaktari ni uhusiano wa kinyanyasaji. Pale ambapo mwenye nguvu, ambaye ni rais anawahujumu na kuwanyanyasa wanyonge ambao ni madaktari. Kando na hayo, msanii anapotuonyesha mwanamke anayeonekana akisema kuwa, hii imekuwa ndoa ya unyanyasaji anatueleza kuwa kuna jambo lisilo la kawaida linajitokeza katika uhusiano wa madaktari na serikali ya rais na naibu rais.

Kwa kawaida ndoa huwa kati ya watu wawili wanaopendana na wameamua kuishi pamoja kwa upendo. Mwanamume anapaswa kumpenda mkewe na mwanamke anapaswa kumheshimu mumewe. Hivyo, msanii anapotusawiria ndoa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685

ambayo mwanamke anachapwa na mumewe, msanii anatusawiria hali ya mnyonge kunyanyaswa na mwenye nguvu. Kwa kifupi, msanii natumia mbinu ya analojia kulinganisha uhusiano kati ya madaktari na serikali ya rais na naibu rais na ndoa yenye unyanyasaji kwa minajili ya kuweka wazi suala la unyanyasaji wa wafanyikazi na hatimaye kumtashtiti kwa kutowajali wanafanyikazi wake.

**Mwingiliano Matini**

Wamitila (2002), anafasili dhana ya mwingiliano matini kama inayotumiwa kuelezea kuwepo kwa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi fulani. Kwa kifupi hapa ni pale sifa za kazi fulani zinajitokeza katika kazi nyingi. Kwa mfano, pale ambapo kuna wimbo katika tamthilia au riwaya fulani. Katika utafiti hii, iligunduliwa kuwa msanii alitumia mbinu hii ya mwingiliano matini, kama njia ya kufichua udhaifu wa viongozi wa Kenya kwa njia ambayo ilikuwa fiche. Mtafiti alikumbana na vibonzo vilivyobeba ploti za riwaya zingine kwa minajili ya kutashtiti uongozi wa nchi ya Kenya. Suala hili lilijitokeza katika Kibonzo $K_4UO$, ambapo msanii amemsawiri mmoja wa wagombeaji wa kiti cha ugavana cha Kaunti ya Nairobi akiwa na pua ndefu. Kwa kawaida, inachukuliwa kuwa mtu mwongo anasemekana kuwa ana pua refu ama husawiriwa akiwa na pua lilio refu kuliko kawaida. Wazo hili lilitokana na riwaya ya watoto; "*Adventures of Pinocchio*" iliyochapishwa nchini Italia na Carlo Collodi katika mwaka wa 1883. Hadithi hii ya Pinocchio ilihusu mwanamme mmoja maskini aliyetaka kijichongea kikaragosi cha mbao ili aweze kupata mtaji wake kutokana na kikaragosi kile.

**Kibonzo 6: $K_4UO$ kinyang'anyiro cha ugavana katika Kaunti ya Nairobi**




Kutoka: (http://gadocartoons.com/nairobi-gubernotorious-race/).

Inasemekana kuwa ubao aliotumiwa kuchongea kikaragosi kile haukuwa wa kawaida na ulikuwa wa kimaajabu. Baada ya kikaragosi kile kuchongwa kilitamani kuwa mvulana halisi aliye hai. Hatimaye, ndoto ya kikaragosi kile ilitimia na akawa hai. Lakini kwa kuwa kilikuwa kimeundwa kwa ubao wa kimaajabu kila kiliponena uongo pua lake lilirefuka. Hatimaye, kutokana na hadithi ile ya Pinocchio, watu walianza kuhusisha mtu mwongo na pua refu. Hivyo, msanii alitumia hadithi ya Pinocchio kuelezea kuwa mgombeaji mmoja wa kiti cha ugavana cha Kaunti ya Nairobi alikuwa ni mtu mwongo na hivyo msanii anaonekana kutia dosari na kumtashtiti mgombeaji yule kwa kwa mtu mwongo. Hivyo basi, msanii akitumia mbinu ya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685

mwingiliano matini katika kibonzo $K_4UO$ kama mbinu ya kuibua maudhui ya kitashtiti na pia kama njia ya kutashtiti uongozi wa nchi ya Kenya.

**Matumizi ya Rangi**

Katika uwanda wa mawasiliano ya ishara, rangi ni mojawapo wa viambajengo muhimu. Matumizi ya rangi katika kazi yoyote ile ya kisanaa, hutumiwa kama mbinu ya mawasiliano yenye nia ya kuleta maana matilaba zaidi ya yale yanayoonekana. Brewer (1994), anaeleza kuwa kwa miaka mingi rangi zimetumika katika sekta mbalimbali kuleta maana mbalimbali. Kwa mfano, katika uchoraji wa ramani, rangi ya kijani kibichi kutumika kuashiria msitu, na rangi ya samawati hutumika kuashiria ziwa. Katika sekta ya hospital kuna msemo kama vile *code blue* ambayo hutumika kuashiria kuwa kuna tukio la dharura linalohitaji matibabu ya haraka kama vile; mshtuko wa moyo au mgonjwa anapoacha kupumua. Kwa kiasi kikubwa, vibonzo vilichapishwa katika tovuti ya Gado vilikuwa vya rangi nyeupe na nyeusi isipokuwa vichache tu vilivyokuwa vimetumia rangi mbalimbali zilizokolezwa. Hivyo, mtafiti alichukulia kuwa kuna ujumbe ambao msanii alikuwa ananunia kupitisha kwa kutumia rangi mbalimbali. Kwa mfano, katika kibonzo $K_3UF$, tunaona msanii atusawiria rais akifungua chupa inayotoa mvuke wa rangi ya kijani kibichi.

**Kibonzo 7: K3UF Majini yametoka kwenye chupa #Unyakuzi wa Ardhi**

Kutoka: (**www.gadocartoons.com**).

Mvuke ule wa kijani kibichi ulikuwa na nyuso za watu maarufu na waliokuwa na uhusiano wa aina fulani na rais wa wakati huo. Baadhi ya sura zilizoonekana katika mvuke ule ni pamoja na aliyekuwa rais wa kwanza wa jamhuri ya kenya ambaye alikua babake mzazi wa rais wa mwaka huo wa 2013, rais wa pili na wa watatu wa nchi ya Kenya ambao walikuwa ni marafiki wa karibu wa rais. Kando na hayo, tunaonyeshwa uso wa naibu rais ambaye sio tu rafiki yake rais bali pia ni naibu wake. Kwenye upande wa kulia wa kibonzo hiki, rais anaonekana ni kana kwamba ameshtuka. Kutokana na usawiri uliopo katika kibonzo hiki, mtafiti anajiuliza, mbona Gado akaamua kutumia mvuke wa kijani kibichi kuelezea suala la unyakuzi wa ardhi na washukiwa wake?

Katika kemia, gesi inayotoa rangi ya kijani kibichi ni gesi ya klorini. Kwa kawaida gesi hii ina harufu mbaya na inachukuliwa kuwa yenye sumu na ina mmenyuko wa hali ya juu. Hivyo, Gado ametumia ishara ya gesi ya kijani kibichi kudhihirisha kuwa waliotajwa kwenye kesi za unyakuzi wa ardhi ni watu mashuhuri waliostahili kulinda sheria na mali ya umma, na isitoshe ni watu wenye uhusiano wa karibu na rais. Kwa hivyo, wanapotajwa kwenye kesi za unyakuzi wa ardhi linakuwa ni jambo lenye mmenyuko kwani rais mwenyewe anaweza akajipata katika tuhuma hizi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685

za wizi wa ardhi ikiwa baba yake mzazi yupo ndani na pia naibu wake. Kutokana na maelezo haya, tunaona kuwa msanii Gado alitumia mvuke wa rangi ya kijani kibichi, kuelezea suala la unyakuzi wa ardhi za umma kama jambo ambalo rais hangeweza kutatua kwani hata yeye mwenye alikuwa kwa njia moja au nyingine amehusishwa nalo. Kwa kudokezea sifa za gesi ya klorine kupitia mchoro huu, msanii alikuwa anamtashtiti rais kwa kujifanya kuwa angesuluhisha swala la unyakuzi wa ardhi ilhali yeye mwenyewe alifaidika kutokana na unyakuzi wa ardhi za umma.

**Matumizi ya Alama Speshieli**

Wakati mwingine, wanavibonzo hutumia alama speshieli kama vile, alama ya nyota, mviringo au alama ya reli kwa minajili ya kuelezea yasiyoweza kuandikea kwa wazi. Aghalabu alama hizi hutumika kuonyesha utukano au maneno yanayochukuliwa kuwa pujufu. Kwa mujibu wa utafiti huu, ilidhihirka kuwa msanii alitumia mbinu hii kuonyesha ukosefu wa maadili wa baadhi ya viongozi wa nchi ya Kenya na kwa kuwasawiri kwa njia hiyo, alitaka kuweka wazi upungufu wao ili kuwakebehi na kuwatashtiti. Hali hii inajitokeza katika kibonzo $K_3$UWM ambapo msanii anatuonyesha rais akiwa kwenye mkutano wa kudhibiti hasira na Gado ametumia alama za reli, nyota, na mviringo kuwakilisha maneno ya matusi.

**Kibonzo 8: $K_3$UWM Mkutano wa Kusaidia Kudhibiti Hasira**

Kutoka: (**www.gadocartoons.com**).

Katika kibonzo hiki, msanii alikuwa akituelezea matukio yaliyotokea kwenye mkutano wa ziara ya rais katika Kaunti ya Turkana nchini Kenya. Rais alikuwa ameenda kuzindua mradi wa uchimbaji mafuta katika eneo la Tulow. Gavana Nanok alipotoa hotuba yake, alimrai rais kuhakikisha kuwa asilimia kubwa ya faida inayotokana na uchimbaji wa mafuta katika eneo lile ibaki kwenye kaunti hiyo na asimilia iliyosalia ipashwe kwenye serikali ya kitaifa.

Rais alikerwa na matamshi ya Gavana Nanok na akatamka maneno haya;

"Mtu akisimama hapa aseme ati Uhuru ako na haja na mafuta ya wengine. **Ashindwe shetani mshenzi...**si mimi napitisha sheria. Kazi yangu ni kupitisha kidole halafu **mjinga** anakuja hapa kusema... Wa kufikiria mimi ni mtu wa kutishwa watafute mwingine. Mimi shida yangu sio uongozi. Mi shida yangu ni kufanya kazi ambayo

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685

itabadilisha maisha ya wananchi. Kwa hivyo wakufikiria mimi ni mtu ya kutishwa watafute mwengine. Kura ni kura na tutakuja kuomba kama wengine...mtupatie mkose kutupatia kwani mnafikiri dunia itaisha." (Muchiri, 2017).

Hivyo katika kibonzo kile, Gado alitumia alama za nyota, heshtegi, na mviringo kuficha matusi ilikolezwa kwa rangi na yaliyotamkwa na rais. Usawiri wa rais kama mtu mwenye hasira na anayeweza tamka maneno ya matusi hadharani ulilenga kumkejeli rais kwa tabia hii na pia kumtashtiti. Hivyo, kutokana na matumizi ya alama speshieli, msanii alifanikiwa katika kuibua tashtiti katika kibonzo kile.

## HITIMISHO

Utafiti huu ulilenga kubainisha mikakati ya kitashtiti inayotumika katika vibonzo vya kisiasa na hasa vile vinanvyochapishwa kwenye mtandao ambako kuna uhuru mwingi wa kujieleza na hapo hakuna udhibiti mkubwa. Kama tulivyokuwa tumedokeza katika utangulizi kuwa mara nyingi tashtiti hufafanuliwa kwa kuangalia ikiwa jambo tunalosema ni la kitashtiti ikiwa linadhihirisha ushambulizi wa aina fulani au uhakiki wa suala fulani kwa minajili ya kuleta mabadiliko au hata kuibua ucheshi.

Kama tulivyodhihirisha kuwa tashtiti haiwezi kufaulu kivyake na aghalabu hutegemea na hutumia mbinu zingine za lugha ili iweze kutambulika. Stinson (2019) anatilia mkazo mawazo ya Knight kwa kudai kuwa ni vigumu kufafanua tashtiti kwa uhakika na kwa kikamilifu, kwa kuwa kumekuwa na vuta nikuvute kuhusiana na ufafanuzi wa tashtiti. Hata hivyo, wataalamu wengi wamekubaliana kuwa tashtiti ni mtindo wala sio utanzu wa fasihi. Katika hali hii, tashtiti huchukuliwa kuwa kimelea. Kutokana na maelezo haya, mtafiti aligundua kuwa tashtiti hutumia mbinu za lugha pamoja na ishara tofuati ili iwezi kujitokeza.

Waaidha, msanii alitumia mbinu za lugha kama vile; kejeli, sitiara, kinaya, analojia, mwilingiliano matini kama mikakati ya kuibua tashtiti katika vibonzo vyake. Kama ilivyokuwa imeelezwa awali, kazi ya tashtiti ni ushambulizi wa wahusika, unaolenga kuleta mabadiliko katika tabia. Hivyo, msanii Gado alikejeli na kukehebi tabia za viongozi waliosawiri katika vibonzo vilivyoteuliwa kwa minajili ya kuleta mabadiliko na kuweka wazi maovu waliokuwa wakitenda Licha ya hayo, uchambuzi na uhakiki wa vibonzo vilivyoteuliwa ulidhibitisha kuwa matumizi ya rangi, msururu wa alama kama vile heshtegi, nyota na mviringo, metonimia, zinaweza kutumika kama mikakati ya kuibua tashtiti katika vibonzo vya kisiasa.

Hivyo, kwa mujibu wa utafiti huu, mtafiti aligundua kuwa msanii Gado alisawiri viongozi wa nchi ya Kenya kama wafisadi, wanafiki, na wenye kukosa maadili. Sababu kuu ya Gado kuwasawiri kwa njia hii ilikuwa ni kuwatashtiti na kuzindua hadhira yake kuhusiana na maovu yaliyokuwa yakiendelea nchini Kenya katika kipindi kile. Pamoja na hayo, msanii alifaulu kwa kutumia mbinu mbalimbali za lugha na ishara mbalimbali kama mikakati ya kuibua tashtiti katika vibonzo vyake.

Isitoshe, mtafiti aligundua kuwa usawiri wa Gado ulisheheni uhuru mwingi wa kujieleza na hakuogopa kuweka wazi maoni yake kuhusiana na kiongozi fulani au suala fulani. Hivyo, sanaa ya Gado ilionyesha ukali na uhuru mwingi katika uangaziaji wa masuala mbalimbali, hali ambayo ni tofauti na vibonzo vinavyochorwa kwenye magazeti ambayo huwa yanafuata sheria fulani za usawiri. Hivyo, utafiti huu ulidhihirisha kuwa uhamiaji wa vibonzo vya kisiasa kutoka magazetini hadi kwenye mitandao ya kibinafsi, ulipelekea kuongezeka kwa makali na uhuru katika usawiri wake. Isitoshe, uhuru na ukali huu ulijitokeza zaidi kutokana na utumizi wa mikakati ya kitashtiti kama vile; kinaya, kejeli, sitiara, analojia, metonimia, mwingiliano matini, matumizi ya rangi na matumizi ya alama speshieli.

## MAREJELEO

Al-Momani, K., Badarneh, M. A., & Migdadi, F. (2017). A semiotic analysis of political cartoons in Jordan in light of the Arab Spring.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685

*HUMOR*, *30*(1). https://doi.org/10.1515/humor-2016-0033

Ayodi, N. K., Beja, S. K., & Ogola, J. O. (2014). Tashtiti na Wanatashtiti: Maana, Umuhimu na Vipengele vyake katika Fasihi. *Mulika*, *33*, 46– 57. https://doi.org/https://journals.udsm.ac.tz/index.php/mj/article/view/1535

Barasa la Kiswahili la Zanzibar. (2010). *Kamusi La kiswahili fasaha*. Oxford University Press.

Brewer, C. A. (1994). Color use guidelines for mapping. *Visualization in modern cartography*, *1994*(123-148), 7

Chandler, D. (2002) *Semiotics for Beginners*. Aberystwyth: Aberystwyth University

Condren, C. (2023). *Between laughter and satire aspects of the historical study of humour*. Springer International Publishing.

Declercq, D. (2018). A definition of satire (and why a definition matters). *The Journal of Aesthetics and Art Criticism*, *76*(3), 319–330. https://doi.org/10.1111/jaac.12563

Dörner, A., & Porzelt, B. (2016). Politisches Gelächter. Rahmen, Rahmungen und Rollen bei Auftritten politischer Akteure in satirischen Interviews desdeutschen Fernsehens. *M&K Medien & Kommunikationswissenschaft*, *64*(3), 339-358.

Eko, L. (2015). The art of satirical deterritorialization: Shifting cartoons from real space to cyberspace in Sub-Saharan africa. *International Communication Gazette*, *77*(3), 248– 266. https://doi.org/10.1177/1748048514568759

Gamen, I. (2022, March 16). *Metonimia Ya Kuona ni Nini?* Creativos Online. https://www.creativosonline.org/sw/Visual-metonymy.html

Griffin, D. (2015). *Satire a critical reintroduction*. The University Press of Kentucky.

Kahigi, K. K. (2020). Sitiari katika Kichomi – Uchambuzi wa Mojawapo ya Mbinu za Kifasihi ya Euphrase Kezilahabi. *Swahili Forum*, *27*, 32–56.

Kondowe, W., Fishani Ngwira, F., & Madula, P. (2014). Linguistic Analysis of Malawi Political Newspaper Cartoonson President Joyce Banda: Towards Grice's Conversational Implicature. International Journal of Humanities and Social Science, 4(7), 40-51.

Knight, C. A. (2004). *The literature of Satire*. Cambridge University Press.

Lichtenstein, D., & Nitsch, C. (2022). Content analysis in the research field of satire. *Standardisierte Inhaltsanalyse in Der Kommunikationswissenschaft – Standardized Content Analysis in Communication Research*, 277– 286. https://doi.org/10.1007/978-3-658-36179-2_24

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi Ya Fasihi*. Standard Textbooks Graphics and Pub.

Muchiri, M. (2017, March 9). *Shock as Uhuru calls politician 'Shetani Mshenzi' in public [video]*. Kenyans.co.ke. from http://www.Kenyans.co.ke/news/president-Uhuru-Kenyatta-bitter-exchange-words-turkana-governor-josphat-nanok-17370

Mulanda, O., & Telewa, V. K. (2014). In the Cartoonist's Mind: Exploring Political Comic Strips in Kenyan Daily Newspapers. *The Journal of Pan African Studies, Vol.6, No.9, May 2014*, *6*(9), 30–40.

Mwetulundila, R., & Kangira, J. (2015). An Analysis of Rhetoric and Humour in Dudley's Political Cartoons Published in the Namibian Newspaper in 2012. *International Journal of Research in Humanities and Social Sciences*, *2*(6), 63–75. https://doi.org/ ISSN 2394-6296 (Online)

Ng'etich, K. K. (2020). The Power of Satire: an analysis of Gado's Cartoons in The Standard

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1685

newspapers (Unpublished master's dissertation). Aga Khan University, East Africa.

Peifer, J., & Lee, T. (2019). Satire and journalism. *Oxford Research Encyclopedia of Communication*. https://doi.org/10.1093/acrefore/9780190228613.013.871

Salisu Ogbo, U., & Nuhu, M. (2016). Satire as tool of political cartoons in the Nigerian National Dailies: A Critical Discourse Analysis. *European Scientific Journal, ESJ*, *12*(29), 124. https://doi.org/10.19044/esj.2016.v12n29p124

Sani, I. (2014) 'The use of verbal and visual metaphors in the construction of satire in Nigerian political cartoons', *Online Journal of Communication and Media Technologies*, 4(2). doi:10.29333/ojcmt/2471.

Sani, I., Abdullah, M.H., Ali, A.M & Abdullah, F.S. (2012). The role of humour in the construction of Satire in Nigerian political cartoons. *Online journal of communication and media technologies,2(3),* 148-153.

Stinson, E. (2019). Satire. *Oxford Research Encyclopedia of Literature*. https://doi.org/10.1093/acrefore/9780190201098.013.1091

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.